

HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

MKOA WA RUKWA
TEL: +255 2802429
FAX: +255 2802796
Mob: +255 622 858 482
Email ded@kalambodc.go.tz
Website: www.kalambodc.go.tz



S.L.P 3,
MATAI,
KALAMBO
TANZANIA

Unapojibu tafadhali taja:

24/05/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo amepokea kibali cha ajira mpya toka kwa Katibu Mkuu OR - Utumishi chenye Kumb. Na. FA.97/228/01/9 ya tarehe 13/05/2022, Hivyo napenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa kutuma maombi kwa nafasi nne (4) kama ifuatavyo:-

1. Madereva II (Nafasi 3)
2. Katibu Mahsusi III (Nafasi 1)

DEREVA DARAJA LA II - NAFASI (3)

- Awe amehitimu kidato cha Nne (IV)
- Awe na leseni ya Daraja la E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanya kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- Awe na cheti cha Majaribio ya ufundi Daraja la II

KAZI NA MAJUKUMU YA DEREVA

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari.
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
- Kufanya usafi wa gari na
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake.

NGAZI YA MSHAHARA - TGS B

KATIBU MAHSUSI III - NAFASI (1)

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe amehitimu kidato cha Nne (IV)
- Awe amehitimu mafunzo ya Uhaziri na kufaulu mtihani wa hatua ya tatu
- Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kingereza maneno 80 kwa dakika moja.
- Awe amepata mafunzo ya kompyuta katika chuo chochote kinachotambulika na Serikali na kupata cheti katika program za **Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.**

KAZI NA MAJUKUMU YA KATIBU MAHSUSI III

- Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
- Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba za kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anayofanyia kazi, na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka, au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini
- Kusaidia kufikisha maelezo ya mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
- Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maofisa waliokatika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

NGAZI YA MSHAHARA - TGS B

MASHARTI YA JUMLA

- Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
- Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa
- Mwombaji aambatanishe maelezo yake binafsi yaliyojitosheleza (CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za simu.

- Maombi yaambatanishwe na picha moja (Passport size) ya hivi karibuni na iandikwe jina kwa nyuma.
- Barua za maombi ziandikwe kwa mkono na ziambatanishwe na nakala za vyeti vya elimu na taaluma kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.
- **Testimonials, Provisional results, Statement of result** hazikubaliki.
- waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimefanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE.
- Waombaji wote watapaswa kuangalia mara kwa mara kwenye tovuti ya Halmashauri kwani wale watakaoitwa kwenye mchujo wa awali majina yatawekwa hapo.
- Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo
S.L.P 3
KALAMBO

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **05/06/2022** saa 9:30 Alasiri

Imetolewa na


Shafi K. Mpenda

Mkurugenzi Mtendaji (W)

HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
KALAMBO**

NAKALA;

Katibu,

Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,

Jengo la Utumishi (UDOM),

Eneo la Dkt. Asha Rose Migiro,

Sanduku la Posta 2320,

DODOMA

Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo www.kalambodc.go.tz

Mbao za matangazo